

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

Simu No: 0654-258282
0652-576221

SHULE YA SEKONDARI LIKONGOWELE
S.L.P 10,
LIWALE.

14/12/2020.

MZAZI/ MLEZI

**YAH: KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI YA
LIKONGOWELE**

Hongera, kwa kuchaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Likongowele kwa mwaka 2021. Unashauriwa kutumia vyema nafasi hii uliyopewa na taifa kwa ustawi wako binafsi, familia yako na Taifa kwa ujumla.

KURIPOTI SHULENI:

Ripoti shuleni tarehe **11/01/2021 siku ya Jumatatu** bila kukosa, ili uwahi mafunzo ya kiingereza yatakatolewa mara tu baada ya masomo ya kidato cha kwanza kuanza.

**SARE YA SHULE
WAVULANA**

- Mashati 2 rangi nyeupe (mikono mifupi).
- Suruali 2 rangi ya kahawia (isiwe modo).
- Suruali 2 rangi nyeusi (isiwe modo).
- Nguo za michezo–bukta rangi yoyote na T.Shirt rangi ya zambarau, pamoja na viatu vya michezo.
- Mkanda mweusi wa ngozi.
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba (gidamu)

WASICHANA

- Mashati 2 rangi nyeupe (mikono mifupi).
- Sketi 2 rangi kahawia ndefu ivuke magoti.
- Kiatu cheusi chenye kamba na kisigino kisiwe kirefu.
- Nguo za michezo-sketi rangi nyeusi na T.Shirt rangi ya zambarau, pamoja na viatu vya michezo.
- Hijabu inaruhusiwa kwa anaye hitaji. Lakini iwe ya heshima na sio kubwa sana.

MAHITAJI YA DARASANI

- Daftari 10 kubwa/counter.
- Kamusi ya kiingereza kwa Kiswahili.
- Kalamu za wino nyeusi au bluu, penseli na mkebe wa Hisabati.
- Rimu ya karatasi kwa ajili ya mitihani ya kila wiki na mwezi.

.....
E . J. MOSES
MKUU WA SHULE

SHERIA ZA SHULE

Zifuatazo ni sheria za shule:-

Kwenda kinyume na sheria hizi kutampelekea mwanafunzi kuadhibiwa na hatimaye kufukuzwa shule. Tafadhali zisomwe kwa makini na mwanafunzi pamoja na mzazi/mlezi ili zieleweke vizuri.

A. MAKOSA YA KUFUKUZWA SHULE

1. Wizi.
2. Uasherati, ubakaji na ushoga.
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyaa.
4. Uvutaji wa bangi.
5. Makosa ya jinai.
6. Kupigana na kupiga.
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
8. Kudharau Bendera ya Taifa.
9. Kuoau au kuolewa.
10. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
11. Kutoa mimba.
12. Kugoma , kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu.
13. Kukataa adhabu kwa makusudi.

B. YAFUATAYO YATEKELEZWE NA MWANAFUNZI KINYUME CHAKE NI KUADHIBIWA.

1. Aheshimu wakubwa na wenzake.
2. Akimbie mara baada ya kuitwa na mwalimu au mlezi awapo shuleni.
3. Atii kengele na kufuata ratiba vizuri.
4. Avae sare na mavazi mengine kwa heshima.
5. Aombe ruhusa kabla ya kuondoka shuleni.
6. Aonane na kuongea na wageni baada ya kupata ruhusa ya mwalimu wa zamu au mlezi husika.
7. Awe mtiifu kwa viongozi wa serikali, shule na serikali ya wanafunzi (viranja).
8. Awepo darasani wakati wote wa vipindi na ashiriki katika kazi zote za usafi au za mikono.
9. Aongee lugha ya kiingereza wakati wote wa masomo yake hapa shuleni.
10. Awe milinzi na mtunzaji wa mali ya umma.
11. Kuheshimu na kukubali tofauti za kisiasa, kidini na kiutamaduni
12. Kuwa msafi wakati wote.
13. Kuthamini muda “ muda ni mali”.
14. Kunyoosha mkono juu na kusimama wakati wa kuuliza au kujibu maswali.
15. Kuwahi shuleni kwa tarehe zilizopangwa.
16. Kuheshimiana wao kwa wao na wengine walioko ndani na nje ya mazingira ya shule.

